JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

SIRI

Simu Na: +255 (026) 2963630
Nukushi: +255 (026) 2963629
Barua Pepe: ps@utumishi.go.tz
Tovuti: http://www.utumishi.go.tz



Menejimenti ya Utumishi wa Umma
na Utawala Bora,
Jengo la Taaluma Na. 1,
Chuo cha Masomo ya Biashara na Sheria,
Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),
Barabara ya Mkalama,
S.L.P. 670,
40404 DODOMA.

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. CFC. 26/205/01"Y"/56

06 Juni, 2017

Makatibu Wakuu
Makatibu Tawala wa Mikoa
Wakuu wa Idara za Serikali Zinazojitegemea
Wakurugenzi wa Majiji, Manispaa na Miji
Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Wilaya
Watendaji wa Taasisi za Umma
Watendaji Wakuu wa Wakala za Serikali
TANZANIA BARA

YAH: ZOEZI LA KUHAKIKI WATUMISHI WA UMMA KWA KUTUMIA TAARIFA ZA KITAMBULISHO CHA TAIFA PAMOJA NA UKAGUZI WA UINGIZWAJI WA TAARIFA ZA VITUO VYA AFYA NA ELIMU KATIKA MFUMO WA HCMIS

Kama mnavyokumbuka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) ilifanya zoezi la kuwasajili watumishi wa Umma nchi nzima kwa ajili ya kuwapatia Namba ya Utambulisho na Kitambulisho cha Taifa kuanzia mwezi Septemba, 2016 hadi mwezi Machi, 2017. Kazi hii kwa sasa imekamilika ambapo taarifa za watumishi 495,700 waliosajiliwa na kupatiwa Kitambulisho cha Taifa au Namba ya Kitambulisho cha Taifa (National Identification Number – NIN) zimekwishachakatwa na kuingizwa kwenye Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS). Hatua inayofuata ni kufanya uhakiki wa taarifa za watumishi wote wa Umma kwa kutumia taarifa za NIDA zilizoingizwa kwenye Mfumo wa HCMIS.

2. Ili kufanikisha zoezi hilo, mafunzo kwa Maofisa Utumishi kuhusu uhakiki wa watumishi kwa kutumia taarifa za NIDA pamoja na zoezi lenyewe la uhakiki yamepangwa kufanyika kwa taasisi zote za Serikali kati ya tarehe 12 Juni hadi 15 Julai, 2017. Zoezi hili litawahusisha maofisa kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na

SIRI

Downgraded

Scanned by CamScanner

Utawala Bora (OR-MUUUB) pamoja na Maofisa Utumishi kutoka taasisi zote za Serikali. Kazi zitakazofanyika katika kipindi hicho ni pamoja na:-

a) Kutoa mafunzo kwa Maofisa Utumishi walioteuliwa kutoka taasisi zote kuhusu matumizi sahihi ya fomu na ripoti za NIDA zilizojengwa kwenye mfumo wa HCMIS pamoja na matumizi ya fomu ya kuingiza taarifa za Kiapo cha Maadili;
b) Kutoa maelekezo na utaratibu wa namna ya kufanya zoezi la uhakiki wa watumishi kwa kutumia taarifa za NIDA kwa Maofisa Utumishi kutoka katika taasisi zote;
c) Kusimamia zoezi la uhakiki wa watumishi kwa kutumia taarifa za NIDA, zoezi ambalo litafanywa na Maofisa Utumishi waliopatiwa mafunzo na;
d) Kuendelea na ufuatiliaji wa moja kwa moja wa utekelezaji wa mfumo wa HCMIS katika vituo vya kutolea huduma (Service Delivery Points – SDPs) katika Idara za Elimu na Afya.

3. Mafunzo kwa ajili ya Maofisa Utumishi wa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa yatafanyika kwa siku moja katika Ofisi za Makatibu Tawala wa Mkoa husika. Mafunzo kwa ajili ya Wizara na Taasisi zilizopo Dar es Salaam na Dodoma yatafanyika kwa siku moja katika Ofisi ya OR-MUUUB, Dar es Salaam na Dodoma. Aidha, kwa taasisi nyingine zilizopo katika mikoa mingine, Maofisa Utumishi wa taasisi hizo watapatiwa mafunzo katika Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa husika. Kila mwajiri atateua na kuwagharamia maafisa Utumishi wawili (2) au zaidi kulingana na wingi wa watumishi aliyonayo. Waajiri wote watajulishwa tarehe mahususi ambayo mafunzo tajwa yatafanyika.

4. Baada ya mafunzo hayo, zoezi la uhakiki wa watumishi litaanza mara moja kwenye kila taasisi na litatekelezwa na Maofisa Utumishi waliopata mafunzo . Ili kufanikisha zoezi hili kwa wakati, watumishi wote wa Serikali ambao vituo vyao vya kazi vipo nje ya makao makuu ya **Taasisi** zao watahakikiwa katika Wilaya wanazofanyia kazi chini ya usimamizi wa Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ambako zoezi hili litafanyika. Aidha, kila mtumishi atapaswa kuwa na nyaraka zifuatazo wakati wa uhakiki:-

(a) Kitambulisho cha kazi chenye picha ya mtumishi husika;
(b) Hati ya malipo ya mshahara (Salary slip) na;
(c) Kitambulisho cha Taifa au Namba ya Utambulisho wa Taifa.

5. Maofisa kutoka OR-MUUUB watatembelea kila mwajiri kwa ajili ya kukagua utekelezaji wa zoezi hilo. Sambamba na zoezi uhakiki, pia Maoafisa wa OR-MUUUB watafanya ukaguzi kuhusu ufanisi wa matumizi ya Mfumo wa HCMIS katika sehemu za kutolea huduma

Scanned by CamScanner

...Ps) katika Idara za Elimu ya Sekondari, Msingi na Afya katika ...amlaka za Serikali za Mitaa.

6. **Taasisi zitakazohusika na zoezi hili ni zile ambazo watumishi wake wanalipwa mishahara kupitia Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS). Utaratibu wa kuwahakiki watumishi wengine wanaolipwa mshahara nje ya Mfumo huu utatolewa na Msajili wa Hazina**. Ni matumaini yangu kwamba **mtashiriki na kusimamia** ipasavyo utekelezaji wa zoezi hili ili liweze kukamilika katika muda uliopangwa.

Ninawashukuru kwa ushirikiano wenu.

Dr. Laurean d. Ndumbaro
KATIBU MKUU (UTUMISHI)

Nakala: Msajili wa Hazina,
Ofisi ya Msajili wa Hazina,
S.L.P 3193,
DAR ES SALAAM. {Tafadhali andaa utaratibu wa kuhakiki watumishi wanaolipwa mshahara nje ya Mfumo wa HCMIS na kuwajulisha}.

Scanned by CamScanner